

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1  
Nukushi: 255-262961502  
Barua pepe : [press@ikulu.go.tz](mailto:press@ikulu.go.tz)  
Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)



OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,  
CHAMWINO,  
S.L.P 1102,  
40400 DODOMA.

*Mtwara*  
*15 Septemba, 2023*

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**RAIS SAMIA AANZA ZIARA YA KIKAZI MKOANI MTWARA**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amewataka wasafirishaji wa korosho kwa malori mkoani Mtwara kupata kibali maalum kutoka kwa Mkuu wa Mkoa huo.

Rais Samia amesema hayo wakati akihutubia wananchi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika uwanja wa Nangwanda Sijaona.

Aidha, Rais Samia amesema lengo la kibali hicho ni kuweza kupata takwimu sahihi za korosho zinazosafirishwa kutoka mkoani humo kwani wapo wafanyabiashara wanaokwepa kusafirisha kwa njia ya bandari.

Rais Samia ameagiza kutumika kwa eneo maalum bandarini lililotengwa kwa ajili ya kupitisha korosho na nafaka nyingine kwa kuwa halitumiki ipasavyo kwa kisingizio cha uchafuzi unaosababishwa na makaa ya mawe.

Rais Samia amemuagiza Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe kuwashughulikia wafanyabiashara wanaochakachua korosho njiani wanaposafirisha kwa malori kwa minajili ya kupata faida kubwa ambapo huathiri ubora wa korosho kwenye soko la dunia.

Kwa upande mwingine, Rais Samia amezitaka Kamati za Ulinzi na Usalama za mikoa nchini kushughulikia na kuipa kipaumbele migogoro ya wakulima na wafugaji katika maeneo yao.

Awali, Rais Samia alikagua miradi ya maendeleo ikiwemo uzinduzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini, chujo la maji la Mangamba, ukarabati wa kiwanja cha ndege, barabara ya Mtwara-Mnivata (km 50) na kukagua shughuli za uimarishwaji wa bandari.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Zuhura Yunus'.

Zuhura Yunus  
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

